



SWIS-H
STATEWIDE INFANT
SCREENING - HEARING



NILICHAGUA KUTOPIMA UWEZO WA KUSIKIA WA MTOTO WANGU. NAHITAJI KUJUA NINI?

Mtoto wako atatolewa mfululizo wa uchunguzi wa afya katika wiki chache za kwanza za maisha yake. Mmojawapo wa huu ni kuchunguza kupoteza uwezo wa kusikia.

Uchunguzi wa kusikia utatolewa haraka iwezekanavyo baada ya kuzaliwa na unaweza kufanywa hospitalini kabla au baada ya kuruhusiwa kutoka hospitali, au kwa mahali pa jamii pa eneo.

Wazazi wanaweza kukataa kutoa ruhusa ya uchunguzi wa uwezo wa kusikia wa mtoto mchanga wao. Hii itaandikiwa katika Kumbukumbu ya Afya ya Kibinafsi (Kitabu cha Bluu) ya mtoto wako. Pia utaombwa kuweka saini katika fomu kuhakikisha kwamba ulikataa uchunguzi ulipokutolewa.

Ukichagua kutopata uchunguzi wa mtoto wako, bado ufahamishwe kuhusu uchunguzi na umuhimu wake.

KWA NINI UCHUNGUZI WA KUSIKIA UNATOLEWA?

Wastani wa mtoto mmoja au watoto wawili katika kila watoto 1000 wanaozaliwa watapata kupoteza uwezo wa kusikia wa maana.

Ni muhimu kugundua haraka iwezekanavyo jinsi mtoto wako anavyoweza kusikia ili wewe na mtoto wako muweze kupata ushauri sahihi na msaada.

Wakati watoto wanaposema neno la kwanza wameshakuwa wanasikiliza jinsi tunavyosema kwa kadiri ya mwaka mmoja.

Kama mtoto hasikii vizuri mnamo wakati huu, maendeleo yao ya matamshi na lugha yanaweza kuathiriwa.

Ukitaka habari zaidi au ukibadilisha wazo lako na utake mtoto wako kupimwa, wasiliana na mratibu wa mradi SWIS-H wa eneo lako haraka iwezekanavyo.

NAHITAJI KUFANYA NINI MTOTO WANGU ANAPOKUA MKUBWA ZAIDI?

Kusikia kunaweza kutoendelea sawasawa wakati ukipita. Ni muhimu kufuatia maendeleo ya matamshi na lugha ya mtoto wako pamoja na majibu yao ya sauti.

Unaweza kutumia orodha ya kukagulia upande wa nyuma ya karatasi ili kufuatilia maendeleo ya mtoto wako.

Ukiwa unahangaika kusikia au maendeleo ya matamshi na lugha ya mtoto wako baadaye, tafadhali fanya mpango wa kupima kusikia kwa mtoto wako. Omba daktari wako wa familia kukurejeza kwa huduma inayofaa ili kupima kusikia kwa mtoto wako.

Kusikia kunaweza kupimwa kwa umri wowote.

KWA MAELEZO ZAIDI TAFADHALI UANGALIE TOVUTI IPO CHINI:

<http://www.health.nsw.gov.au/kids-families>

Habari za miadi/wasiliano wa eneo

Kwa ushauri wa afya wasiliana na *healthdirect Australia*
<http://www.healthdirect.gov.au/>

1800 022 222





ORODHA YA KUKAGULIWA KWA KUSIKIA

Kuzaliwa mpaka miezi 3	Huvutiwa na sauti kubwa
	Hunyamaza akisikia sauti alizozoea
	Hufanya sauti za kulia polepole kama njiwa
	Huvutiwa na kusema kwa kuangalia uso wa msemaji
Miezi 3-6	Hugeuza macho au kichwa kuelekea upande wa sauti
	Huanza kufanya sauti zinazoiga kusema
	Hucheka na anafanya sauti kuonyesha jinsi anavyojihisi
Miezi 6-9	Huropokwa 'dada', 'ma-ma' 'baba'
	Hupiga kelele/sauti ili kuvuta macho
	Hujibu mara nyingi kwa 'hapana' na jina lake lenyewe
	Huvutiwa na kuimba na muziki
Miezi 9-12	Huiga sauti ya kusema ya wengine
	Huelewa maneno ya rahisi, km 'mpira' 'mbwa' 'baba'
	Hugeuza kichwa na kukielekeza kwa sauti nyororo
	Husema maneno ya kwanza
Miezi 12-18	Inaonekana anafahamu maneno mapya zaidi kila wiki
	Hufuata maelekezo ya rahisi ya kusema, km 'leta mpira'
	Huonyesha kuelekea watu, viungo vya mwili au vitu akiulizwa
	Huendelea kujifunza maneno mapya ya kusema ingawa labda si wazi
Miezi 18-24	Huna kati ya maeneo 100-200 anayetumia kila mara
	Husikiliza hadithi na nyimbo rahisi
	Huunganisha maneno mawili au zaidi kuwa kifungu kifupi km 'jusi zaidi'

Ukumbusho:

